HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI NYOLOLO
S.L.P 382-MAFINGA
10/12/2020

Kumb.Na.Nyoss/JOIN/VOL.1/2020
Jina la Mwanafunzi……
S.L.P ……
……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYOLOLO KIDATO CHA KWANZA 2021

1.0 Ninayofuraha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha kwanza kwa mwaka 2021.Shule ya sekondari Nyololo ipo umbali wa km 7 kaskazini magharibi kutoka Nyololo Njiapanda.Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021,unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 07/01/2021 saa 1:30 asubuhi kwa ajili ya kuandikishwa.Shule ni ya kutwa kwa wavulana tu na hosteli kwa wasichana wote .

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

1. WASICHANA

A. Sketi mbili (02) zinazovuka magoti,zenye rinda 10 tu rangi ya kijani(**01**)na rangi ya "**dark blue**"(**01**)(istim No.1)(**sampuli ya kitambaa imeambatanishwa katika fomu hii)**
B. Shati moja (01) nyeupe ya mikono mirefu na tisheti moja(**itapatikana shuleni**)
C. Tai ya kijani inayofanana na rangi ya sketi
D. Soksi nyeupe ndefu pea 02
E. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba viwe na kisigino kifupi(**jozi mbili**)
F. Sweta rangi ya kijani (isiwe kijani ya jeshi)
G. Hijabu rangi nyeupe (kwa waislamu tu)
H. Track suit ya bluu na raba kwa ajili ya michezo
N.B Nguo zisizo za heshima hazitakubalika

2. WAVULANA

I. Shati moja (01) nyeupe ya mikono mirefu na tisheti moja(**itapatikana shuleni**)
ii. suruali 2 ya kijani **(01)** na dark blue **(01)** zenye pindo chini(turn up)
(**sampuli ya kitambaa imeambatanishwa katika fomu hii)**
iii.Mkanda mweusi kwa ajili ya suruali
iv. Tai 1 ya kijani inayofanana na rangi ya suruali
v. Soksi nyeusi pea 02
vi. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba viwe na kisigino kifupi(jozi mbili)
vii. Sweta rangi ya kijani (isiwe kijanijeshi)
viii. Bukta na T-Shirt rangi ya bluu na raba hivi ni kwa ajili ya michezo

NB: Suruali fupi na zinazobana (modo) hazitapokelewa

2.2 VIFAA VYA TAALUMA

A. Daftari kubwa (counter books)quire 2 (09) kwa ajili ya masomo darasani
B. Kamusi ya lugha ya kiingereza (English Dictionary)
C. Kalamu za kutosha
D. Faili lenye gamba gumu la kutunzia mitihani yake (box file)
E. Mfagio[chelewa] na kindoo cha lita kumi kwaajili ya usafi wa mazingira ya shule

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

3.1.Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongazo yote inanyotolewa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

.

Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo

a. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri darasani na katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kiukamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare za shule wakati wote uwapo shuleni.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kutunza mali za umma.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule mara moja.

a. Wizi
b. Uasherati,ubakaji,ushoga ulawiti na usagaji.
c. ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika
d. kupigana au kupiga.
e. kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
f. kudharau bendera ya taifa.
g. kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
h. kuoa au kuolewa
i. kutoa mimba.

j.Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k.Kukataa adhabu kwa makusudi-
l.Kuwa na simu ya mkononi au kumiliki laini ya simu.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

A. Medical examination form(fomu ya hospitali)ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali/kituo cha afya ya /cha /serikali.fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

B. Soma kwa makini na kujaza fomu ya kukubali kujiunga na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……..
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI NYOLOLO,
S.L.P 382,
MAFINGA.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYOLOLO

JINA LA MWANAFUNZI……..
KIDATO CHA KWANZA MWAKA…….

TAMKO LA MZAZI/MLEZI

1. Mimi ……mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.Nakiri kuwa nimeelewa maelezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu ajiunge na shule hii na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wote kama ilivyoagizwa kwenye fomu ya kujiunga na shule.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ilikufanikisha malengo yake.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo ya taaluma yake muda wote awapo shuleni na nyumbani.
5. Naahidi kusimamia mahudhurio yake shuleni na kutoa taarifa kwa walimu endapo ameshindwa kufika shuleni.
6. Naahidi kuwa endapo sitatoa ushirikiano kama nilivyo ahidi hatua za kisheria zinifuate.

JINA LA MZAZI/MLEZI……
ANUANI YA MZAZI/MLEZI…….
NAMBA YA SIMU……

TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi……niliyechaguliwa kujiunga na shule hii,naahidi kuwa mtiifu kwa sheria za shule na kuwa na nidhamu,kujituma kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa wenzangu,ikiwa nitafanya tofauti na niliyoahidi nichukuliwe hatua dhidi ya kanuni na sheria za shule.

JINA LA MWANAFUNZI……

SAHIHI……
TAREHE…….

MUFINDI DISTRICT COUNCIL
NYOLOLO SECONDARY SCHOOL
STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

To be complete by a government medical officer and returned to the **Headmistress NYOLOLO SECONDARY SCHOOL**

REF……

Please examine the student named above and comment on his/her health by responding to the following items.

Kindly put a mark (v) in front of **YES** or **NO**

Does the student have problems in connection with

A. Sight?.....1.NO
2.YES

If yes state……..

B. Hearing?.....1.NO
2.YES

If yes state……..

C. Chest (lungs)……1.NO
2.YES

If yes state……

D. Blood pressure……1.NO
2.YES

If yes state……..

E. Any physical disability……1.NO
2.YES

If yes state……..

Do you there recommend the said student medically fit for studentship at this school?.....

If NO, please state…….....

……

NAME …….……..

……..

DESIGNATION

SIGNATURE ……..